# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, naomba kutanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu aliyetuumba, kutujaalia uhai na uzima wake uliotuwezesha kupata fursa hii adhimu na muhimu ya kukutana katika Mkutano huu wa Saba kwa lengo la kuwatumikia wananchi pamoja na kutekeleza jukumu letu muhimu lililoelezwa katika kifungu cha 88(b) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuhusiana na kazi moja kuu ya Baraza la Wawakilishi ya kupitisha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati ya PAC kuwa na jukumu la kuchambua na kutafakari ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini pia ina jukumu jengine la kujadili bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 107, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020).

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilitekeleza jukumu hilo kwa kukutana na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali siku ya Jumamosi ya tarehe 23 Aprili, 2022 kwa ajili ya kujadili pamoja na kuchambua utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2021/2022 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoainishwa katika Fungu E04 la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hata hivyo, Kamati ya PAC imegundua kasoro mbali mbali ambapo Kamati yetu imeweza kutoa ushauri mahsusi katika maeneo yanayohusika na kasoro hizo ili Bajeti ya Ofisi hii iweze kutekelezeka ipasavyo na kuleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC ilipokuwa ikipitia taarifa za kibajeti za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iligundua kuwepo kwa kasoro katika taarifa zinazohusiana na Watendakazi waliopo na wanaohitajika. Kamati ya PAC ilichunguza kwa undani taarifa hizo kwa kufanya mlinganisho na taarifa za kibajeti za Wizara ya Fedha na Mipango ambazo zilipitishwa na Baraza lako mwaka 2021/2022 na kugundua kuna utofauti wa tafsiri ya neno ‘wanaohitajika’ pamoja na utofauti katika

uainishaji wa idadi ya watendakazi wanaohitajika katika Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilitafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo kutoka kwa watendaji wa Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango lakini Kamati haikuridhika na maelezo yaliyotolewa na kushauri kwamba watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara wa Fedha na Mipango wakae pamoja ili waweze kulijadili na kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa mantiki ya kuwa na mfumo mmoja wa kuripoti taarifa za kibajeti za watendakazi zinazowiana baina ya Taasisi moja na nyengine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC ilipokuwa ikipitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 kuhusiana na shughuli ya ulipaji mishahara wafanyakazi wake, iligundua kwamba Ofisi ya Mdhibiti (CAG) imetumia asilimia 110 kwa ajili ya ulipaji mishahara ya wafanyakazi wake na kuelezwa kwamba hilo limetokana na kuthibitishwa kwa muundo mpya wa utumishi wa Ofisi hiyo na kusababisha watendaji wanne kuteuliwa kuwa Wakurugenzi jambo ambalo liliongeza matumizi ya fedha za mishahara zilizopangwa awali. Sambamba na hilo, kulikuwa na wafanyakazi tisa (9) waliorudi Ofisini kutoka masomoni ambao waliogezewa mishahara na posho.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu iliridhika na majibu yaliyotolewa na watendaji na kuishauri Ofisi hiyo kwamba maelezo au sababu hizo ni za msingi, Hivyo, ni busara zikaelezwa katika Hotuba yao ya bajeti ili iweze kutoa taswira halisi ya kile kilichotekelezwa na Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeanzisha utaratibu mpya wa ulipaji tozo za ukaguzi kwa Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitazolipwa kulingana na uwezo na hadhi ya Taasisi husika, wakati awali Ofisi ya CAG, ilikuwa inatumia kiwango kimoja (flat rate) cha malipo cha shilingi milioni sita (6,000,000/-) kwa kila Taasisi ambacho kilikuwa kinatumika katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, iwapo utaratibu mpya wa utonzaji tozo za ukaguzi utatumika na kusimamiwa ipasavyo, Kamati yetu ina matumaini kwamba mapato ya CAG yataongezeka maradufu kwani kuna Taasisi zimeweza kutathminiwa kuwa na uwezo wa kulipa hadi milioni (17) kutoka milioni Sita (6) waliyokuwa wakilipa awali. Kamati ya PAC, inaishauri Ofisi ya CAG kufanya kazi kwa bidii zaidi na kusimamia kikamilifu ulipaji wa tozo hizo ili mapato yake yazidi kuongezeka katika mwaka wa fedha 2022/2023 na kuondokana na changamoto ya kukusanya fedha kidogo za asilimia 24.5 kwa miezi tisa ya bajeti ya mwaka huu tunayoendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC imeendelea kusikitishwa na kilio cha siku nyingi cha kupatiwa bajeti ndogo Ofisi ya CAG isiyokidhi mahitaji muhimu ya utekelezaji wa kazi zake za msingi. Kwa kipindi cha miezi tisa yaan Julai 2021 hadi Machi 2022, Ofisi ya CAG imepatiwa asilimia 43.48 ya matumizi mengineyo. Kutokana na fedha hizo kuwa kidogo, Ofisi ya CAG imeshindwa kutekeleza baadhi ya kazi zake muhimu ilizojipangia.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya CAG inatakiwa iwapatie mafunzo watendaji wake ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya ukaguzi yanayotokea ulimwenguni. Kwa bahati mbaya, Ofisi hii ilishindwa kuwawezesha wafanyakazi wake kushiriki katika mafunzo elekezi yanayohusiana na kutengeneza miongozo ya ukaguzi kupitia vitengo vya 'Technical Support Unit' pamoja na 'Quality Audit Unit' ambayo yaliendeshwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT) katika Mkoa wa Dodoma kwa muda wa wiki mbili. Ukosefu wa fursa hiyo kwa wafanyakazi wa Ofisi hii, kumewakosesha kupata ujuzi stahiki utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao kitaalamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa muongozo wa Kimataifa wa Taasisi za usimamizi wa Ukaguzi za AFROSAI na INTOSAI, inazitaka Taasisi za Ukaguzi kuwa Wakala wa Bunge katika masuala ya ukaguzi. Hivyo, Ofisi ya CAG inalo jukumu kubwa la kuhakikisha inaziwezesha Kamati za Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa kuzipatia mafunzo ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na ufanisi unaohitajika na umma. Kutokana na kupatiwa fedha kidogo, Ofisi ya CAG hushindwa kulitekeleza jukumu hilo na kushindwa kufikia vigezo vilivyowekwa na Taasisi hizo za Kimataifa kwani hutakiwa kwa uchache kutoa mafunzo si chini ya siku 15 hadi 30 kwa Kamati za kifedha. Kutokana na changamoto hiyo, Ofisi ya CAG siku zote hushindwa kufikia kigezo hicho na kutia doa katika uwezo wa utekelezaji wa shughuli zake kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC inaishauri Serikali ama kuiongezea bajeti Ofisi hii itakayokidhi mahitaji yake ya ndani na nje au kuandaa utaratibu wa kuingiza fedha maalum Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ili ziweze kutumika kwa ajili ya kuwawezesha watendaji wa CAG kuzipatia mafunzo Kamati zetu za Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali hasa ukizingatia ugumu uliopo wa kufanya uchunguzi kwa mambo ambayo yanaweza kumuwajibisha kiutendaji muhusika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imegundua kwamba Ofisi ya CAG imesaini makubaliano 'Memorandum of Understanding (MoU)' na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania ya kushirikiana kufanya Ukaguzi Jumuishi katika Balozi tofauti ambazo Tanzania imeweka Mwakilishi wake ndani na nje ya Nchi zilizomo katika Bara la Afrika. Kupitia makubaliano hayo, Watendaji wa Ofisi hizo mbili zinashirikiana wakati wa kufanya mipango ya ukaguzi huo pamoja na uandaaji wa ripoti husika. Hata hivyo, kila Taasisi huwa inajitegemea katika bajeti ya kuwawezesha wafanyakazi wake kuweza kushiriki katika ukaguzi huo.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa azma hiyo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliwapatia taarifa Ofisi ya CAG mara kadhaa kwamba wamekusudia kufanya ukaguzi katika Balozi saba lakini Ofisi ya CAG ilishindwa kulitekeleza hilo kwasababu bajeti yao ilikuwa haikidhi.

**Mheshimiwa Spika,** Lakushangaza na kusikitisha, katika mpango wa bajeti ya mwaka huu, Ofisi ya CAG ilipanga shughuli (activities) tatu za kusafiri nje ya nchi ili kutekeleza

lengo la ukaguzi katika Balozi za Tanzania lakini haikuweza kufanya hivyo kutokana na upungufu wa fedha. Mheshimiwa Spika, kutoshiriki katika ukaguzi huo, kunaipelekea Taasisi hiyo kusuasua katika utekelezaji wa makubaliano yaliyopo pamoja na kushindwa kutoa ripoti ya Ukaguzi Jumuishi kuhusu mapato na matumizi yanayofanywa na Ofisi hizo kwani tufahamu kwamba hizo ni Ofisi za Serikali na zinatumia rasilimali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania, Ofisi ya Mdhibiti inalo jukumu la kufanya Ukaguzi Jumuishi katika Miradi ya Maendeleo ambayo inatekelezwa kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022, Ofisi ya CAG ilikusudia kufanya ukaguzi katika maeneo tofauti. Hata hivyo, kutokana na changamoto za kibajeti, Ofisi ya CAG ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa Mradi wa Maendeleo wa TASAF katika Mkoa ya Arusha na Mradi wa MKURABITA katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kufanyika kwa Ukaguzi Jumuishi katika maeneo yaliyopo nje ya Zanzibar kutazipatia fursa Kamati zako za Kifedha kuanzisha utaratibu wa kushirikiana na Kamati za kifedha za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kuifuatilia kwa pamoja ripoti itakayotolewa kutokana na Ukaguzi Jumuishi huo ili kujua thamani halisi ya fedha za wananchi zilivyotumika katika Balozi au Mikoa hiyo. Hivyo, kutokuwa na bajeti ya kutosha katika Ofisi ya CAG ni kuzikosesha haki yake ya kikanuni Kamati zako za kifedha. Kwa mantiki hiyo, kuna kila sababu kwa Serikali kuiangalia kwa jicho la karibu bajeti ya CAG ili ziweze kwenda sambamba na dhana nzima ya utekelezaji wa Ukaguzi Jumuishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC imegundua kwamba katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023, Ofisi ya CAG haikupangiwa fedha katika Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti inayopatikana katika kifungu kidogo cha SE040203 ambapo katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kilikuwa na jumla ya shilingi milioni 335,872,000 zilizopangwa kwa kazi hiyo. Kamati yetu ilitaka kujua shughuli hiyo itatekelezwa vipi wakati fedha zake hazikupangwa na kuelezwa kwamba kwa kipindi cha mwaka ujao, shughuli za uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itatekelezwa moja kwa moja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na haitokuwa katika bajeti yao. Kamati yetu inasisitiza kwamba pamoja na fedha kuingizwa katika Wizara lakini shughuli hizo ziendelee kutekelezwa kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni haya yanayohusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoandaliwa na Wajumbe wa Kamati yetu. Kwa umuhimu wa kipekee, na kwa ruhusa yako, naomba sasa nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe na makatibu wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Juma Ali Khatib - Mwenyekiti;
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Makamu Mwenyekiti;
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe;

4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe;
5. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe;
6. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Mjumbe;
7. Ndg. Maryam Haji Ali - Katibu; na
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine, naomba kuchukua nafasi hii kutamka kuwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) imeyakubali Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2022/2023. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muiunge mkono bajeti hii, ili ile mipango mizuri iliyopangwa iweze kutelekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC), naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



…………………
Mhe. Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.